

UKIUSHI KAMA ELEMENTI YA KIMTINDO KATIKA BAADHI YA RIWAYA ZA KEN WALIBORA

Mercy Moraa Motanya.

Chuo Kikuu cha Kabianga, Kenya

Emmanuel Kisurulia.

Chuo Kikuu cha Kabianga, Kenya

Salim Sawe.

Chuo Kikuu cha Kabianga, Kenya

©2021

**International Academic Journal of Social Sciences and Education (IAJSSE) | ISSN
2518-2412**

Received: 1st July 2021

Published: 7th July 2021

Full Length Research

Available Online at: https://iajournals.org/articles/iajsse_v2_i2_340_353.pdf

Citation: Motanya, M. M. Kisurulia, E., Sawe, S. (2021). Ukiushi kama elementi ya kimtindo katika baadhi ya riwaya za Ken Walibora. *International Academic Journal of Social Sciences and Education*, 2(2), 340-353

IKISIRI

Makala haya ni uchanganuzi wa ukiushi kama elementi ya mtindo kwenye riwaya nne za Kiswahili zilizoandikwa na Ken Walibora kutumia mkabala wa kiisimu. Isimu ni taaluma inayochunguza lugha kwa kuzingatia taratibu za kisayansi. Uchanganuzi wa data ambao ulitumiwa ni wa kimaelezo na uliongozwa na nadharia ya umitindo. Nadharia hii ina nguzo za kuchanganua kazi za fasihi kwa misingi ya kiisimu na hubainisha kanuni za kuelezea uteuzi uliofanywa na mwandishi katika matumizi yake ya lugha kuhusu mambo ya kijamii, utoaji na upokeaji wa maana,

uhakiki wa kidiskosi na ule wa kifasihi. Lengo mahsusi ni kuchanganua aina za ukiushi katika riwaya nne za Ken Walibora. Sampuli iliteuliwa kimaksudu na data ilikusanywa kwa njia ya kusoma vitabu husika na kisha kudondoa mifano mwafaka na kuinakili kwa ajili ya kutoa maelezo kulingana na lengo la utafiti huu. Makala haya ni muhimu kwa kuwa yameweka wazi namna waandishi wa riwaya za Kiswahili wanavyotumia ukiushi kama elementi ya mtindo wa kiisimu ili kuwasilisha ujumbe wao katika kazi za fasihi.

Maneno muhimu: Isimu, ukiushi, umitindo, diskosi, riwaya

UTANGULIZI

Mtindo ni sifa muhimu inayobainisha kazi nzuri na kazi duni ya fasihi na humwezesha mwandishi wa kazi ya fasihi kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake. Mtindo umefafanuliwa na Wamitila (2003) kuwa ni sifa maalumu za mwandishi au mazoea ya mwandishi fulani ambayo hujionyesha kwenye fani yake, mazoea hayo ya mwandishi ya kuandika, kuteua msamiati, tamathali za semi, taswira, uakifishaji, sentensi na kadhalika ndio yanayompambanua mwandishi mmoja na mwingine. Wamitila anaendelea kusema kuwa mtindo unahusu namna mwandishi anavyoiunda kazi yake na huweza kutumiwa kwa misingi hiyo kuonyesha sifa zake maalum au mazoea yake yanayoonekana katika kazi zake za uandishi. Kwa jinsi hiyo, mtindo huifanya kazi ya mwandishi kutambulika. Kwa kauli hii yake, tunaweza kusema kwamba mtindo wa mwandishi fulani hauwezi kujulikana kwa kusoma kazi yake moja tu bali upekee wa mwandishi huweza kubainishwa baada ya kupitia kazi zake kadhaa.

Ukiushi, kwa mujibu wa Cluysenaar (1976), ni kuondoka katika maana inayotarajiwa kwa kuzingatia viwango tofauti vya lugha kama vile semantiki, leksika, sarufi, mofolojia, fonolojia na grafolojia. Viwango hivyo mbalimbali vinaweza kuwa katika sarufi na fonolojia au katika viwango vya sentensi na virai. Ukiushi unaweza kuashiria ukuaji wa utanzu wa fasihi anavyosema Mohamed (1986). Hii ni kwa vile utanzu wa fasihi unaopitia ukiushi kila uchao haubaki vile vile wakati wote. Ukosefu wa ukiushi huweza kuwafanya waandishi wote wafanane wakati wote katika uandishi wao au ukasababisha utanzu ukose mvuto kwa sababu ya kutobadilika kwa sababu kuna kiwango cha mabadiliko yanayosababishwa na ukiushi. Hii inaashiria kuwa waandishi wa riwaya ya Kiswahili wasipoendeleza ukiushi huu, riwaya haitageuka, haitabadilika wala kupiga hatua. Ukiushi ndio moyo wa ubunifu utakaodumisha

uhai katika riwaya na ulitotoa kutoka jana, ukatuleta leo na unatuelekeza kwenye kesho ya utunzi. Ukiushi huzaa upya hata kama ni upya wa kurudiwa au wa kukopwa.

Msingi wa Nadharia

Nadharia ya umitindo iliasisiwa mwaka wa 1904 na Viktor Shyklovsky alipogundua kuwa lugha hutumika kwa njia inayofanya mambo ya kawaida kuonekana mapya. Leech (1969) anasema kuwa umitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma, unaofungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haujisimamii kivyake. Msamiati mpana wa kimsingi katika uhakiki wa kifasihi hususan taswira, kinyume, kinaya, kejeli, usambamba na jazanda hauwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana za kiisimu kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Umitindo huangazia matumizi ya dayolojia au mazungumzo yanayohusisha lafudhi zinazotambulisha maeneo ya kijiografia na lahaja za wazungumzaji wa eneo fulani, lugha elezi na sarufi kwa mfano sajili au rejista, sauti, aina za sentensi na kadhalika. Kimsingi, nadharia hii inaweza kuchunguza mtindo wa kinachosemwa au kuwasilishwa na jinsi kinavyowasilishwa. Tumeitumia nadharia hii katika kuchambua aina za ukiushi katika riwaya nne za Ken Walibora kwa sababu kupitia kwa dayolojia, tunapata ukiushi unaotokana na mambo kama vile athari za lugha ya kwanza na mazoea ya matumizi ya lugha katika jamii.

Mbinu za Kukusanya Data

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani ili kupata data kulingana na malengo yake na mihimili ya nadharia iliyochaguliwa. Vitabu vya fasihi vilivyoteuliwa kwa minajili ya mada hii ni pamoja na *Siku Njema* (1996), *Kufa Kuzikana* (2003), *Ndoto ya Almasi* (2006) na *Kidagaa Kimemwozea* (2012). Vitabu hivi vilichanganuliwa ili kupata data iliyofaa utafiti huu. Uteuzi wa sampuli katika utafiti huu ulikuwa wa kimakusudi ambapo riwaya nne za Ken Walibora zilichaguliwa. Aina sita za ukiushi zilishughulikiwa ili kuweka wazi ukiushi kama elementi ya mtindo uliotumiwa na Ken Walibora katika riwaya zake zilizochaguliwa ili kuafikiana na malengo ya utafiti huu. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya kusoma na kuchambua riwaya zilizoteuliwa kulingana na lengo la utafiti huu.

Matokeo

Utafiti huu unaonyesha jinsi aina mbalimbali za ukiushi wa kiisimu zilivyotumiwa katika kuendeleza mtindo wa kazi zilizoteuliwa. Aina za ukiushi ambazo zimeshughulikiwa ni ukiushi wa kifonolojia, wa kimofolojia, ukiushi unaotokana na athari za lugha ya kwanza, wa kisarufi (ukiushi wa kisintaksia na kisemantiki) na ukiushi wa kiisimu matini.

Aina za Ukiushi Katika Riwaya Nne za Ken Walibora

Ukiushi wa kifonolojia

Fonolojia ni tawi la isimu ambalo hujishughulisha na mfuatano wa sauti katika kuunda silabi, mfuatano wa sauti katika kuunda mofu na hatimaye mfuatano wa mofu katika kuunda maneno (Massamba, Kihore na Msanjila, 2004). Matumizi ya lugha kwa kawaida huhusisha uteuzi wa fonimu zinazotumiwa ili kuunda maneno au msamiati maalum. Fasihi hutumia lugha kujieleza ambapo vipengele vinavyohusishwa katika uteuzi huu ni vingi kikiwepo kiwango cha fonimu. Ukiushi wa kifonolojia hushughulikia mambo kama vile kudondosha au kuongeza fonimu katika neno kwa madhumuni ya kuwasilisha ujumbe na kudhihirisha mtindo wa mwandishi.

Udondoshaji wa fonimu au silabi kwenye umbo la neon

Mwandishi aliteua kutumia udondoshaji wa fonimu ili kusawiri jinsi mazungumzo ya kawaida ya mhusika katika riwaya hubadili maumbo ya maneno. Udondoshaji huu wa fonimu hudhihirisha ukiushi katika umbo la neno. Mifano ifuatayo inaonyesha ukiushi wa kifonolojia kama mtindo wa Ken Walibora wa kutumia maneno yaliyofupishwa kwa kudondolewa kwa fonimu ili kuleta mvuto kwa hadhira yake. Maneno kama vile 'likenda', 'meokoka', na 'kashika', yanafaa kuwa 'likaenda', 'nimeokoka', na 'ameshika au akashika'. Ken Walibora ametumia udondoshaji huu wa silabi ili kudhihirisha ukiushi wa kifonolojia.

Mifano 1a) *Kidagaa Kimemwozea*

i. *Gari la Mtemi **likenda** na kutokomea kwenye upeo wa macho.(uk74)*

Mfano (1b) *Ndoto ya Almasi*

*Mimi 'meokoka kama file wewe **nahubiri** neno.(uk 133)*

Mfano (1c) *Kufa Kuzikana*

*Mmojawapo wa wanawake hao alikuwa **kashika** mikongojo huku na huku na miguuni alikuwa na kikandiko kilichoufunika unyayo na kifundo cha mguu.(uk43)*

Mfano (1d) *Siku Njema*

*"Shoti **nende** mjomba," nikasema kwa mkazo...Ningekuruhusu **wende wendako**...(uk39)*

Kushirikishwa kwa sifa hizi za kudondosha silabi katika neno huchangia kuonyesha ukiushi wa kifonolojia katika kazi za Ken Walibora kwa wasomaji wake. Mifano hii inaashiria kwamba ukiushi unatumika kama sehemu ya mtindo katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili.

Matumizi ya kipekee ya sauti

Kazi za mwandishi zinaonyesha matumizi ya sauti moja moja au misururu ya fonimu. Matumizi maalum ya sauti huchangia kuendeleza upekee wa kazi ya mwandishi. Ken Walibora alichagua kutumia misururu ya konsonanti pekee katika kujenga umbo ‘Sssh’ (mfano 2i), jambo ambalo si la kawaida katika Kiswahili ili kuwasilisha maana ya kunyamaza. Hii inamaanisha kuwa ametumia mtindo huu kama ukiushi wa kaida za uundaji wa maneno ya Kiswahili kwa sababu ya mazoea ya kutumia maneno hayo katika jamii. Hii ni kwa vile angetumia neno ‘nyamaza’ lakini badala yake aliamua kutumia msururu wa konsonanti kimtindo. Uteuzi huo huchangia uhai wa kazi ya mwandishi. Kwa mfano:

Mfano (2) **Kufa Kuzikana**

i) “**Sssh.**” *Tim aliniashiria ninyamaze. (uk30)*

ii) *Nimebaki pale na A, E, I, O, U yangu ya shamba. (uk19)*

Ken Walibora ametumia ‘A, E, I, O, U’ kiukiushi katika matini yake. Hii ni kwa vile, ingawa sauti hizi tano ni foni tu ambazo hazijatumika kuunda neno halisi la kimofolojia, katika mfano (2ii), kisemantiki foni hizo zinabeba maana ya kimtindo ya kutojua mambo mengi au kuwa na ujuzi mdogo wa mambo.

Matumizi ya Akronimi

Uchunguzi wa kazi za Walibora zilizolengwa uliashiria pia kwamba huwa anatumia akronimi kama fonimu zinazowakilisha umbo la neno. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, anatumia sauti mbili ‘TV’ kama kifupisho cha televisheni badala ya neno la Kiswahili ‘runinga’. Kwa mujibu wa makala haya, hapana budi kwamba Ken Walibora alikuwa anajua vibadala viwili vya Kiswahili, ‘runinga’ na ‘televisheni’, ambavyo angetumia badala ya ‘TV’ ila alifanya uteuzihuu kuonyesha jinsi usemi huu umezoeleka kutumika katika jamii ambamo anaandika. Jambo ambalo linaashiria mtindo wake kupitia kwa ukiushi.

Mfano 3a) **Kufa Kuzikana**

i. “**TV crew ya SK watafika hapa punde,**” *alinong’ona bwana mmoja mfupi mwenye kitumbo kilichotokeza mbele. (uk 47)*

Mifano 3b) **Kidagaa Kimemwozea**

i. **ITT-Idhaa ya Taifa ya Tomoko (uk26)**

ii. **DJ(uk7-10)**

iii. **SLP Uk 49**

iv. **Songoa FC uk 56**

Matumizi ya herufi ‘TV’ na ‘SK’ katika muktadha kwenye mfano (3a ii) katika ukurasa (47) wa riwaya ya *Kufa Kuzikana* yanashadidia ukiushi wa umbo la maneno katika mtindo wa mwandishi. Hata hivyo, maana ya ‘SK’ (crew ya SK) si wazi katika muktadha wenyewe hasa kwa wasomaji licha ya kutumika kwake. Mifano (3b) ni akronimi ambazo maana yazo inajulikana lakini zimezoelewa kutumika kwa ufupi katika jamii anamoandikia kazi zake.

Ukiushi wa Kimofolojia

Leech na Short (1981) wanasema kwamba ukiushi wa kimofolojia unahusu kueleza masuala ya ukiukaji katika namna maneno yanavyoundwa, maumbo ya maneno yasiyo ya kawaida kwa mujibu wa kanuni za lugha, mnyambuliko wa maneno usio sahihi miongoni mwa masuala mengine ya kimofolojia. Ukiushi huu unaonyesha uhuru wa mwandishi wa kuzua miundo ya ruwaza fulani inayosababisha ‘unadra’ au upekee fulani jinsi anavyoita Chapman (1973).

Utenzishaji kiushi

Utenzishaji kiushi ni dhana inayorejelea hali ambapo mwandishi anaunda vitenzi katika kazi zake kwa kutumia maneno ambayo kwa kawaida huwa hayatumiwi kama vitenzi ila labda ni nomino, vivumishi au hata vielezi. Ken Walibora ameweza kutumia mtindo huo wa kugeuza nomino kama vile ‘nafasi’ na kuitumia kujenga kitenzi ‘nafasika’ kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

Mfano (5a) *Kufa Kuzikana*

- i. *Katika mojawapo ya barua hizo ndipo aliponialika kumtembelea jijini pindi nikinafasika (uk10)*
- ii. *Nimehongera (uk15)*

Mifano (5b) *Ndoto ya Almasi*

- i. *Labda tummithilish na wachezaji wa kandanda waliofungwa bao moja kwenye mechi muhimu na dakika zilizobaki hazikumruhusu kuku kudonoa hata punje moja ya mahindi. (uk131)*
- ii. *Almasi alihamu fursa ya kumbukulia chebosio wimbo mpya aliokuwa anaimba babake.(uk146)*

Mifano (5a i-iv) inaashiria jinsi Ken Walibora anayanyambua maumbo mengine ya maneno ili kuunda kimtindo leksimu zitakazowakilisha maana anayolenga kupitisha kwa hadhira yake. Vitenzi kwenye mifano (5a na 5b) hapo juu vimeundwa kutokana na nomino. Kwa mfano mwandishi ameunda kitenzi ‘nafasika’ kutoka neno nafasi, ‘nimehongera’ kutokana na neno ‘hongera,’ ‘tummithilish’ kutokana na neno ‘mithili’ na ‘alihamu’ kutokana na neno ‘hamu’.

Ukiushi unaotokana na athari ya lugha ya kwanza

Uchunguzi wa matini nne zilizoteuliwa za Ken Walibora umeonyesha mtindo wake unaohusiana na matumizi ya sentensi zilizo na ukiushi unaotokana na athari za lugha za kwanza. Ukiushi huu unahusu uteuzi wa msamiati ambao umekiuka kanuni za Kiswahili sanifu kwa mfano kutumia maneno yaliyoathiriwa na lugha ya kwanza. Hii inamaanisha kuwa mwandishi amejenga sentensi zake kwa kutumia taratibu za kimtindo zinazokiuka kaida za Kiswahili sanifu kuhusu uundaji wa maneno. Mifano (6a) na (6b) inaonyesha matumizi ya lugha yenye ukiushi yaliyoathiriwa na lugha ya kwanza.

Mfano (6a): Siku Njema

- i. Uliniponza nikafungwa **jera**. Sasa nimetoka **jera**. Utakiona cha mutema kuni. **taree** 31 Julai 1971 muaka uu nitakuua. Selemani. (uk33)
- ii. Kongoweya wewe ndiye **ulinihariya** bahati yangu, ulipokimbilia **Mwambasa ulifikili** sitokupata. Nitakuua. Niko **apa** mjini. (Uk100)

Mfano (6b): Kufa Kuzikana

- i. "Wakanjuu mumechokosa nyuki kwa **kumuuwaa** mukoroso. Ama muondoke au mufe muzingani." (Uk 5)

Mifano (6a na 6b) ina leksimu zilizoendelezwa na mwandishi kwa kukiuka miendelezo yao ya kawaida. Hii inadhahirisha jinsi mwandishi anaashiria hali ambapo athari za lugha ya kwanza huathiri uandishi na uzungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Maneno 'muswahili', 'taree', 'jera', 'uu', 'mwambasa', 'ulifikili', 'ulinihariya', 'apa' na 'kumuuwaa' yameendelezwa visivyo. Maneno haya yanafaa kuwa, 'mswahili', 'tarehe', 'jela', 'huu', 'Mombasa', 'ulifikiri', 'uliniharibia', 'hapa' na 'kumuu'. Walibora ametumia mofu zilizoendelezwa vibaya ili kuonyesha ukiushi katika uandishi na kudhahirisha jinsi matumizi ya lugha huathiriwa na lugha ya kwanza ya mzungumzaji. Hali hii huchangia uhai wa riwaya za Walibora kwa sababu katika mazungumzo ya kawaida, wahusika hawajali sarufi bali wanazungumza lugha jinsi wanavyojua.

Mifano zaidi ifuatayo inaendelea kudhahirisha ukiushi unaotokana na athari za lugha ya kwanza katika matumizi ya lugha.

Mfano (7a): Siku Njema

Kumbe wewe unakulanga chai ya stringi?...yaani umeishiko Mombasa ama nini? Ohoo! unajua sisi watu wa para hatuchui Kiswahili kama watu wa pwani. Lakini sisi si watu wapaya. Kama ningekuwa nimeendako mombasa ningechiona kama khale khatoto kha jirani yangu. Watu wanaojua Kiswahili wanajiringanga sana (uk105)

Mfano (7b): Ndoto ya Almasi

"Nasikia watoto wa siku hisi wanapenda kufanya mikomo, kama akuna chumbi...wao nachoma chikoni ya skuli. Upusi kabisa..." (uk38)

Mifano ya (7a na 7b) inaonyesha ukiushi unaochochewa na athari za lugha ya kwanza jinsi watu wa maeneo fulani wanavyokizungumza Kiswahili. Leksimu kama vile 'unakulanga', 'umeishiko', 'para' 'khale khatoto kha...', 'ntiyo', 'mupentwa', 'pwana', 'mikomo' na 'chambasi' zimeathiriwa na lugha ya kwanza au lugha inayozungumzwa na watu kutoka maeneo ya magharibi mwa Kenya. Maneno sahihi ni 'unakua', 'umeishi', 'bara' 'kale katoto ka...', 'ndiyo', 'mpendwa', 'bwana', 'migomo' na 'jambazi'.

Ukiushi wa kisarufi

Sarufi ndiyo nguzo kuu ya maandishi na ni msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matumizi ya lugha kwenye miktadha mbalimbali na hujumlisha viwango vya kimofolojia na kisintaksia. Sarufi hushughulikia mpangilio wa maneno katika sentensi kwa kubainisha visehemu vyake ambavyo huwa na dhima maalum katika kazi zozote za usanii. Ukiushi wa kisarufi huhusisha masuala kama kubananga sarufi, kukiuka kanuni za kutunga sentensi na hata uundaji wa maneno. Kwa ujumla, kiwango hiki huzingatia ukiushi katika muundo wa kawaida wa matumizi ya lugha, urefu wa sentensi (fupi au ndefu) na sentensi zenye dosari, (Leech 1969 na Wamitila 2008)

Ukiushi wa kisintaksia

Wamitilla (2003) anasema kwamba sintaksia hutumiwa kuelezea sehemu ya taaluma ya isimu inayohusika na miundo na mipangilio ya sentensi naye Habwe (2007) anafafanua sintaksia kuwa ni utanzu wa isimu unaoshughulikia muundo wa sentensi na elementi nyingine zinazounda sentensi kama vile maneno na kategoria zake, vikundi na vishazi. Hivyo ukiushi wa kisintaksia unaweza kutokea pale ambapo mwandishi hatazingatia kanuni za kawaida katika utungaji wa sentensi.

Matumizi ya sentensi zisizozingatia sarufi

Sentensi ya kisarufi ni dhana ya kiisimu inayotumiwa kurejelea sentensi inayozingatia kanuni za kisintaksia na kisemantiki. Hii ni sentensi inayokubalika kwa wazawa-lugha kama inayozingatia mpangilio sahihi wa viambajengo na inayobeba maana. Dhana hii hutumiwa kiisimu kurejelea muundo unaorejelewa kwa lugha ya kawaida kama 'sentensi sahihi'. Kando na kule kutumiwa kwa sentensi za kisarufi, Ken Walibora ametumia sentensi zilizokiuka sarufi ambazo zinadhihirisha ukiushi wa kisintaksia. Sentensi zilizokiuka sarufi ni zile ambazo hazijafuata kanuni za kisarufi katika muundo wake lakini maana yake inaeleweka. Lugha ya mazungumzo kwa wakati mwingi huwa na sentensi hizi. Utukiaji huu unaonekana katika mifano (8) ifuatayo.

Mfano(8a) *Kidagaa Kimemwozea*

Ngozi yake, weusi uliokoza. (uk 1)

Mfano (8b) *Ndoto ya Almasi.*

Wakaangua kicheko, kicheko cha kilio. (uk20)

Mfano (8c) *Siku Njema*

Nguvu zikanitindika mwilini, nikawa mchege. (uk 12)

Mfano (8d) *Kufa Kuzikana*

Laiti mama angalikuwepo leo, ashiriki furaha na fahari yangu. (uk 1)

Mifano (8a) na (8b) inaonyesha namna ambavyo mwandishi ametumia mtindo wa sentensi zisizo-sarufi. Hii ni kwa vile katika mfano (8a) aliweka koma baada ya kivumishi 'yake' na kuifanya sehemu ya pili ya sentensi 'weusi uliokoza' kutotimiza kanuni za sarufi. Sehemu hii ya pili ya sentensi ina urejeshi (o), jambo linaloifanya sehemu hiyo kuwa kishazi kitegemezi

ambacho kinahitaji kukamilishwa. Pengine sentensi hii ingekuwa, ‘Ngozi yake ilikuwa na weusi uliokoza’ Mfano wa pili (8b) umekiuka sarufi pale ambapo amerudia neno ‘kicheko’ baada ya kuweka koma baada ya neno ‘kicheko’ la kwanza. Kisarufi, neno ‘kicheko’ halingerudiwa bali sentensi hiyo ingekuwa, ‘Wakaangua kicheko cha kilio.’ Mifano (8c na 8d) ni sentensi fupi ambazo hazihitaji kuwa na koma lakini zimewekwa koma kama sentensi ndefu. Hali hii inaonyesha ukiushi wa kisintaksia. Ingawa sentensi hizi zina upungufu wa kisarufi hasa katika vijenzi vya sentensi, matumizi ya koma yanazifanya zionekane kama zinazozingatia mtindo wa kuandika sentensi kishairi ambapo vijenzi huweza kupanguliwa, kufupishwa na kudondoshwa. Hali hii inaonyesha ukiushi wa kisarufi. Mfano ufuatao unaonyesha usosarufi wa sentensi ambapo ngeli imekiukwa katika kuuliza swali.

Mfano (8e) Kufa Kuzikana

- i. *Dadako gani aliyesoma hata shule ya chekechea?(uk 4)*
- ii. *Aisee hebu tulettee soda. Utakunywa nini? (Uk13)*

Mifano (8e) inaonyesha kuwa mwandishi hajazingatia kiulizi sahihi cha nomino katika sentensi hizi. Nomino ‘dada’ katika sentensi ya kwanza ipo katika ngeli ya *M-Wa* na mwandishi anasema, ‘Dadako gani...’ badala ya ‘Dadako yupi...’ na nomino ‘soda’ katika sentensi ya pili inafaa kuwa na kiulizi ‘gani’ na wala si ‘nini’ Mifano hii inadhihirisha ukiushi wa sintaksia.

Mifano ifuatayo (8f) inaonyesha sentensi ambazo kimaana hazijakamilika na ambazo ni vishazi vitegemezi. Vishazi vitegemezi huhitaji vishazi vingine ili maana ikamilike katika sentensi.

Mfano (8f) Ndoto ya Almasi

- i. *Alitupia jicho kule mbali upande wa matlai, mahali palipokuwa na msitu wa serikali uliofunika vilima vya Cherang’ani. Akaona moshi unafuka. **Michirizimichirizi ya moshi.**(uk4)*
- ii. *Alipokaribia shule ya msingi ya Makutano, matone yalichapuka. Ikawa hasa mvua ya siku za Nuhu, mvua iliyoshitadi kunyesha. Akaamua ataingia kwenye safina pale shuleni; ‘arobaini’ zake zikiisha aendelee na kirago chake cha kuelekea kwao. **Lo! Jinsi ilivyobadilika shule yake ya utotoni!**Aliyatazama majengo ya shule kwa mshangao. (uk4)*
- iii. *Hajui... Hajui atakavyorejesha imani na matumaini ya wazazi wake. Walikuwa na mategemeo makubwa kwa mstakabali wake. **Mtoto wa kiume aliyejaliwa rundo la vipawa.** Sasa amekuwa chanzo cha fedheha na karaha. (uk1)*

Mfano (8f i) ‘Michirizimichirizi ya moshi’ unaonyesha sentensi ambayo haijakamilika lakini mwandishi ameitumia kama sentensi iliyokamilika kimaana. Sentensi hii ni kishazi tegemezi ambacho kinategemea kishazi kingine ili kukamilika kimaana lakini haijakamilishwa bali imewachwa kuning’inia. Mifano (8f ii) na (8f iii) ina vitenzi ambavyo vina ‘o’ ya urejeshi. Sentensi iliyo na kirejeshi huwa na maelezo yaliyo kamilifu inapoongezewa kitenzi kingine kikuu, lakini sentensi hizi hazijakamilika kisarufi ila mwandishi amezitumia kama zilizokamilika. Vitenzi vikiwa na urejeleaji, huwa vinahitaji vitenzi vingine ili sentensi isiwe

kishazi kitegemezi lakini sentensi hizi hazina vitenzi viwili na hivyo basi zinadhihirisha ukiushi wa kisintaksia.

Ukiushi katika sentensi zilizochanganya msimbo.

Kuchanganya msimbo ni ugotanishaji wa vipashio vya zaidi ya lugha moja katika usemi fulani au katika sentensi moja. Hali hii ilibainika katika makala haya kama ukiushi wa kisintaksia unaotumiwa na Ken Walibora katika uandishi wake. Ubadilishaji msimbo hutokea kwa sababu wahusika wanaotumiwa katika matini ni wanawingi-lugha wenye umilisi wa zaidi ya lugha moja na wanazichanganya kwa malengo tofautitofauti, (Buliba Njogu na Mwihi, 2011 na Naseh, 1997). Mfano (9a) unaonyesha jinsi mhusika Mwalimu Majisifu anachanganya lugha ya Kiingereza na Kiswahili ili kuficha ukweli kwamba yeye si mwandishi wa vitabu ila ni kujisifu tu.

Mfano (9a): *Kidagaa kimemwozea*

*“Wataka mimi nipike? Ehee? Ati mimi nalaza damu? wewe unaiamsha damu? **Bloody bastard! I am a writer of distinction.** Hilo yataka ujue... Hakuna mwandishi bora kuliko mimi. Yuko wapi? **no-where.** n'tainyakua mwenyewe **nobel prize for literature** kama sitopewa. (uk 44).*

Ken Walibora ametumia mhusika Mwalimu Majisifu kuonyesha kwamba mtu aliye na ujuzi wa zaidi ya lugha mbili anaweza kuchanganya lugha hizo bila kukiuka kanuni za mojawapo ya lugha hizo anapozungumza. Mhusika huyu anachanganya lugha mbili kwenye usemi wake kwa sababu ya kujionyesha au kujigamba kuwa anafahamu zaidi ya lugha moja kama wanavyosema Iribemwangi na Mukwana (2011).

Katika mifano ya (9b hadi 9d) ifuatayo, Ken Walibora anaonyesha uchanganyaji msimbo ambao ni mtindo unaopendelewa aghalabu na vijana na watu walio na ujuzi wa lugha zaidi ya moja katika mazungumzo yao. Leksimu za Kiingereza zimepachikwa katika sentensi za Kiswahili na kuendelezwa kulingana na kanuni za sentensi za lugha ya Kiswahili.

Mfano (9b): *Kidagaa kimemwozea*

*Basi amu habari za **cousin** zangu? (Uk46)*

Mfano (9c): *Ndoto ya Almasi*

*“Akang’oa **sign post** ya kutangaza shule pale langoni na kuanza kunitandikia”(uk95)*

Mfano (9d): *Kufa kuzikana*

- i. Ungefanya nini na wavamizi wanakuja wakiongozwa na **boss** wako mwenyewe? (Uk 103)*
- ii. “Nikawaona **skin heads** wanne wanamshambulia mwanamke mweusi ...” (uk155)*

Mwandishi ametumia mtindo wa kuchanganya msimbo katika sentensi ili kuonyesha miktadha mbalimbali ambayo hudhihirisha ukiushi unaoleta upekee wake katika kuteua maneno anayoyatumia kwenye uchanganyaji wa msimbo. Leksimu za Kiingereza zimetumika jinsi zilivyo na kufuata kanuni za lugha ya Kiswahili ili kukamilisha usemi katika sentensi

hizo. Maneno kama vile ‘cousin zangu’, ‘sign post ya shule’, ‘boss wako’, yamefuata kanuni za sentensi za Kiswahili ambapo ngeli huzingatiwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa sentensi.

Ukiushi wa kisemantiki

Ukiushi wa kisemantiki unahusisha matumizi ya lugha yanayoathiri maana ya maneno yaliyotumika katika matini. Ukiushi wa aina hii unahusu matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo inavyofasiriwa katika hali za kawaida. Mara nyingi huhusisha matumizi ya maneno kwa njia zisizo za kawaida kimaana, Leech na Short (2007) na Wamitila (2008) wanasema kuwa maana zingine za maneno huwa si wazi na hivyo inabidi msomaji afasiri au kuziwazia kwa undani ili ang’amue ujumbe unaohusika. Ukiushi huu unadhihirisha kuwa neno linaweza kuwa na maana ambayo si ya kawaida au maana ambayo haijazoeleka. Maana hujitokeza katika matumizi yake wala haitegemei jinsi neno linavyojitokeza kwa kuliangalia tu kijuujuu. Matumizi ya lugha yenye maana ya ndani huleta ukiushi wa kisemantiki kwa kuwa maana inayotamkwa siyo inayomaanishwa. Haya yanabainika kwenye mifano ifuatayo.

Mfano(11a)Ndoto ya Almasi

- i. *“Tangu babako kwenda redio haifanyi kazi, haina **makaa**.”*
- ii. *“Rais Kenyatta ametangaza msamaha kwa wafungwa. Nimo miongoni mwa **walioangukiwa na bima**. Vinginevyo ningekuwa bado nasota ndani.”(uk17)*
- iii. *“Naugua mwanangu hali yangu taabani.Lakini nilijua utatoka jela unipate bado **niko sijaenda nyumbani kwa baba**”(uk17)
*“Mama unataka kutuacha?”**
- iv. *“Nawapenda wanangu.Lakini **baba akiniita lazima niitike wito**” (uk 17)*

Maneno yaliyokolezwa kwenye mifano ya hapo juu yanaonyesha ukiushi wa kisemantiki ambapo maneno hayo yamepewa maana tofauti au maana ya ndani. Ukiushi huu humfanya msomaji afikirie na kutafakari maana inayokusudiwa na mwandishi kwenye muktadha huo ili apate kuelewa matini. Maneno kama vile ‘makaa’ limetumika kumaanisha betri au seliumeme lakini mwandishi ameliweka jinsi linavyotumiwa kwenye mazingira ya nyumbani. Vifungu ‘angukiwa na bima’ na ‘sijaenda kwa baba’ vinamaanisha ‘kubahatika’ na ‘sijafariki’ mtawalia. Mifano ifuatayo inaendelea kubainisha ukiushi wa kisemantiki.

Mfano 11b) Kidagaa kimemwozea

- i. *“Sisi kuwa wadosi **mbwa apige mswaki**”(uk10)*
- ii. *“DJ ni mtoto mdogo anayesema maneno yanayomzidi umri,kama mhusika wa riwaya iliyoandikwa vibaya na mwandishi limbukeni, sikwambii lugha yake ya ajabu inayoweza kuwaliza walimu machozi **kikombe tele wakichelea wanafunzi wao kumwiga**”(uk10)*
- iii. *...Mtemi Nasaba Bora alikuwa tayari kumwandalia **ufumbuzi wa kudumu**.(uk13)*

- iv. *Ila baada ya kusifiwa mno na Bi Zuhura, alijikuta kapigwa fagio la chuma na mumewe Bi Zuhura, Mtemi Nasaba Bora, tena bila habari.(uk15)*

Vifungu ‘mbwa apige mswaki’, ‘machozi kikombe tele’, ‘ufumbuji wa kudumu’ na ‘pigwa ufagio wa chuma’ vinamaanisha ‘jambo lisilowezezana’, ‘tatizo kubwa’, ‘kuuawa’, na ‘kufutwa kazi bila malipo’ mtawalia.

Hivyo basi ukiushi wa kisemantiki umetumiwa na Walibora kama mtindo wake ili kutia ladha kwa kazi zake ili zivutie wasomaji wa kazi zake.

Ukiushi wa Kiisimu-Matini

Ukiushi wa kiisimu-matini hutokea pale ambapo kuna matamshi ya kimazungumzo (diskosi) ambayo hayawezi kuainishwa kama maneno au sentensi yanapotokea katika riwaya. Matumizi ya matamko hayo ambayo huwa ni sifa ya mazungumzo yametumiwa na mwandishi ili kuendeleza uhai, mvuto na upekee wa matini yake. Ken Walibora amechagua kutumia tamko kama ‘Sssh’ katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (uk30)* ili kuwasilisha maana ya kunyamaza, jambo ambalo si la kawaida katika matini (maandishi) ila ni la kawaida katika mazungumzo (diskosi). Hii inamaanisha kuwa ametumia mtindo huu kama ukiushi wa kaida. Dayolojia ni sifa kuu ya diskosi ambapo huwa kuna uwezekano wa kuwepo kwa maswali na majibu pamoja na udondoshaji wa sehemu za mazungumzo. Ken Walibora ametumia dayolojia katika riwaya zake nne zilizochunguzwa katika utafiti huu ilihali ni sifa ya tamthilia na kuliko riwaya. Vile inavyoonekana katika mfano ufuatao ulionukuliwa kutoka riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*, ukiushi wa kimatini unadhihirika katika riwaya ya Ken Walibora kwa sababu ametumia sentensi zenye majibizano yenye udondoshaji.

Mfano (12a) *Kidagaa Kimemwozea*

Hiki nacho ni cha nani?” aliuza Amani.

“Cha Fao,” dadake Fao akajibu.(uk 37)

Mfano (12a) unaonyesha ukiushi kwa sababu una dayolojia, una swali na jibu lake na lina sifa ya uwakilishaji kapa au udondoshaji. Amani anauliza swali na dadake Fao anamjibu. Tamko la dadake Fao katika diskosi hii lingekuwa “Hiki nacho ni cha Fao” lakini kwa sababu Amani anafahamu, kipande cha tamko “Hiki nacho ni cha” kinadondoshwa. Ingawa udondoshwaji unaweza kudhihirika katika matini pia, sentensi za riwaya zingetarajiwa kuwa zenye mtiririko kwa sababu ni kazi ya nathari. Usemi kama huu unatumika zaidi katika tamthilia na ukitumiwa katika riwaya, unadhihirisha ukiushi wa kiisimu matini.

Mfano ufuatao pia unaonyesha dayolojia iliyo na ukiushi ambapo wanaelewa wanachokizungumzia na hivyo kutumia nomino au majina mbalimbali wakirejelea mhusika mmoja.

Mfano (12b) *Ndoto ya Almasi*

“Yani yani zimerudi kwetu,” Chebosio alimwambia Almasi.

“Kwa hiyo zinataka redio?”

“Ndiyo.”

“Nguruwe amerudi kugaagaa kwenye upujufu baada ya kuoshwa,”

aliongeza taswira nyingine Almasi. (uk135)

Kutoka kwa mfano huo hapo juu, mhusika anayerejelewa ni Mzee Masasi ambaye ni babake Almasi lakini wahusika wanatumia majina tofauti kumrejelea. Wanatumia ‘yani yani’ na ‘nguruwe’ pengine kwa sababu ya mazoea yake ya kutumia neno ‘yani’ kila wakati ama tabia zake. Mfano huo unaonyesha dayolojia iliyo na udondoshaji wa nomino au jina la mtu ambapo wahusika katika mazungumzo haya wanaelewa. Almasi anaelewa ‘yani yani’ ni nani ndio maana anauliza, “ Kwa hiyo zinataka redio” amedondosha sehemu ya kutaja ‘yani yani’. Udondoshaji huu unaonyesha ukiushi wa kiisimu matini.

Hitimisho

Makala haya yameshughulikia aina sita za ukiushi ambazo ni ukiushi wa kifonolojia, kimofolojia, ukiushi unaotokana na athari ya lugha za kwanza, wa kisarufi ambapo ukiushi wa kisintaksia na kisemantiki na hatimaye ukiushi wa kiisimu matini umeangaziwa. Kupitia kwa ukiushi, wasomaji wa kazi za fasihi wanapata kuburudika, mambo yanapata kuisitizwa, huleta mpatano baina ya riwaya na matini zingine kama vile ushairi na tamthilia, hujenga maudhui ya riwaya na kuchochea hisia za wasomaji na hatimaye ukiushi huficha makali ya mawazo ya mwandishi ili kumfikirisha msomaji. Imedhihirika kupitia kwa mifano iliyodondolewa kutoka baadhi ya riwaya za Ken Walibora kwamba ametumia aina hizi za ukiushi kama mtindo wake wa uandishi. Mwandishi huyu mashuhuri amebobea katika nyanja zote za fasihi hasa utanzu wa riwaya ambapo moja ya riwaya zake, ‘Siku Njema’ inayoshughulikia maswala ya watoto wanaozaliwa nje ya ndoa imetafsiriwa kwa Kiitaliano na Kiingereza.

MAREJELEO

Ahmed, E. B. H. (2015). *Kamusi Teule ya Kiswahili, Kilele cha Lugha*.

Buliba, A. Njogu, K. na Mwihi, A. (2006). *Isimu Jamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Buliba, A. na wenzake (2006) *Sarufi ya Kiswahili: Uchanganuzi na Matumizi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Chapman, R (1973) *Linguistics and Literature: An introduction to Literary Stylistics*. London: Edward Arnold.

Cluysenaar, A. (1976) *Introduction to Literary Stylistics: A Discussion of Dominant Structures in Verse and Prose*. Mishawaka: Pavilion Books

Gathenya, E (2018) Mielekeo na mtindo wa shafi adam shafi Katika riwaya za ‘Kuli’ na ‘Haini’. Tasnifu ya uzamili (hajachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi

- Habwe, J. na Karanja, P. (2007) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Iribemwangi, P. na Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers Limited.
- King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es salaam
- Leech, G.(1969). *A linguistic Guide to English Poetry*. New York: Longman Group Ltd
- Leech, G.na Short, M. (2007). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. Toleo la Pili. Harlow: Longman Group Ltd.
- Massamba, D. Kihore, Y. na Msanjila Y.(2004) *Fonolojia ya Kiswahili sanifu (FOKISA) : sekondari na vyuo*. Dar es salaam: TUKI
- Mohamed, S. (1995) *Kunga za Nathari: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*: Nairobi: East African Educational Publishers
- Walibora, K. (2006) *Ndoto ya Almasi*. Nairobi: Moran Publishers.
- Walibora, K. (2012) *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Target Publications Limited
- Wamitila, K. (2003) *Kichocheo cha Fasihi: Similizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers Limited.
- Wamitila, K. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.
- Wangepi, W. (2018) *Ukiushi wa Kiisimu katika Jumbe Cheshi za Mtandao. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa)* Chuo Kikuu cha Nairobi.